# Our MULTILINGUAL VOICES

Kiangazi 2021 www.houstonisd.com/voices Toleo la I Chapa ya 4

## UJUMBE KWA WAZAZI …

# Safari ya Ghida Hijazi ya Fanaka

Kuhamia Marekani kama mwanafunzi wa shule ya upili ilikuwa safari kuu kwa kuwa nilijua kati ya Kiingereza kidogo na kutojua kabisa. Nilikuwa na wapwa waliohudhuria shule na mimi, ambayo ilifanya mpito kuwa rahisi zaidi. Hata hivyo, changamoto za lugha hazikupotea.



Ghida Hijazi, Mwalimu Mtaalamu, Shule ya msingi ya Cornelius

Darasa la kwanza nililohudhuria lilikuwa la Historia ya Texas. Siku yangu ya kwanza, mwalimu alitupa ramani ya Marekani kama sisimuo na akatuagiza tutambulishe mataifa mengi kadri ya tulivyoyakumbuka. Kwa wakati huo, sikuwa nimewahi kuona ramani nyingine zaidi ya ile ya Lebanon. Niliangalia huku na kule na kuona kila mtu akimalizia mgawo ule, na kwa wakati huo, nilijua nilikuwa tayari kurudi nyumbani.

Nilibahatika kiasi cha haja kuwekwa kwenye programu ya ESL na kupokea msaada kwa madarasa yangu yote. Niliwafahamisha walimu wangu kuwa ningeweza kuelewa karibia 10% ya walichosema. Mazungumzo niliyokuwa nayo na watu shuleni yalikuwa 80% kwa Kiarabu na maneno kadhaa ya Kiingereza niliyoyafahamu. Nilitumia ishara nyingi za mkono mpaka nilipojiamini kuanza kutumia Kiingereza changu.

Kabla ya kujifunza Kiingereza, nilikuwa na msingi imara katika Kiarabu ambayo naamini ilichangia vilivyo katika ustadi wa lugha hizo mbili. Isitoshe, msaada wa walimu niliopata na mfiduo wa daima kwa lugha zote mbili nyumbani na shuleni ilikuwa muhimu katika kuwa mweledi.

Baada ya kuhitimu sekondari, nilihudhuria Chuo Kikuu cha Houston-Downtown na kupokea Shahada ya Sanaa katika Elimu na cheti cha kufunza. Nilifunza ELA kwenye viwango vya kidato cha tatu na cha tano. Nilitambulika kama Mwalimu Mpya wa Mwaka kwenye wilaya mwaka wangu wa kwanza na Mwalimu wa Kiingereza wa Texas wa Mwaka kwenye mwaka wangu wa pili. Ndipo nilipokea shahada ya uzamili katika Utawala na Usimamizi kutoka kwa Chuo Kikuu cha Houston. Nimepitia duara nzima. Nilianza kama mwanafunzi aliyeng'ang'ana kujifunza Kiingereza na kupitia kuwa mwalimu wa ELA, na sasa nawafunza walimu wa ELA jinsi ya kuwapa wanafunzi wetu msaada unaofaa.

Ninawia fanaka yangu kwa wazazi wangu na walimu walioniaminia na kunisukuma niwe toleo langu bora. Wazazi wangu waliacha nyumba yao na familia yao kunileta Marekani kutafuta mustakabali bora. Walitia bidii kunipa nyenzo zote nilizohitaji kufaulu.

Hata kama hawakuweza kunisaidia kiakademia, waliniaminia wakati wote na kunisukuma kuwa bora na hayo yalitosha kunifanya nifaulu.

***Mawaidha ya Bi. Hijazi kwa wazazi:***
Lazima ujue lugha ya kwanza vizuri ili kuweza kujifunza lugha ya pili. Kipande kimoja cha mawaidha ambacho ningewapa wazazi wasiozungumza Kiingereza lakini wangetaka watoto wao kujifunza, ni kuendelea kuwasaidia katika lugha yao ya kwanza ili kujenga msingi thabiti wa kujifunza. Hii itawasaidia kujua lugha ya pili. Wanapaswa vilevile kuwahimiza watoto wao kujizoeza Kiingereza kwa kuzungumza na wazungumzaji asili kadri iwezekanavyo.

**Bi. Hijazi alipoulizwa *Je, "waraka kwangu" yako ingekuwa ipi, ulipokuwa na umri wa miaka 27 kuhusu masomo? Jibu lake lilikuwa: Kujifunza hakuishi! Usiogope kuuliza maswali na kujitoa kutoka pahali pako pa starehe. Huo ndio ufunguo wa fanaka.***

***Ujumbe wake kwa walimu wa HISD:***
Waaminie wanafunzi wako WOTE. Wanaojifunza Kiingereza wana uwezo sawia na wa wanafunzi wengine wote.

## KALENDA YA MITIHANI YA 2020–2021

Kalenda za mitihani za Texas Education Agency (Wakala ya Elimu ya Texas) zinapatikana ili kuhakikiwa. Maelezo ya kutahini ya STAAR/ STAAR Alt na TELPAS/ TELPAS Alt inaweza kufikiwa kwa kubofya https://bit.ly/3psRRov ■

## TONE LA BUSARA



Dkt. Campbell

Ni na furaha kubwa nawakaribisha nyinyi na watoto wenu tena kwenye mwaka wa shule 2021-2022 wa HISD. Hata kama tulikumbwa na mwaka wa shule usio wa kawaida, tulijifunza zaidi kuhusu kuwa na upendo, tulipanua ujuzi wetu, tuligundua kuwa kujifunza kunaweza kuchukua mikondo mbalimbali – kutoka kwa ufunzaji pepe mpaka wa ana kwa ana – na muhimu zaidi, tuligundua jinsi watoto wetu wanavyoweza kuwa imara ajabu. Licha ya kutenganishwa na marafiki na mfumo wao wa kawaida wa mafunzo, wanafunzi wetu walistahimili, na tunajuvunia sana!

Wazazi, nyinyi pia mlikumbwa na wakati wenye msukosuko! Ulikuwa mwalimu ghafla – huku ukiendelea na majukumu ya uzazi. Kama mzazi, najua hii haikuwa kazi rahisi! Tunawashukuru kwa msaada wenu tulipopitia yasiyojulikana.

Tunaazimia mwaka wenye mwanga zaidi – uliojaa furaha na nafasi za kusisimua kwa watoto wetu! Tumeongeza walimu, programu, na makocha kusaidia kazi kazi ya Kitengo cha Programu za Lugha-anuwai, lakini muhimu zaidi, kuwasaidia watoto wetu. Tuna hamu ya kufanya kazi nawe kama mzazi na ujue kuwa tunakuona wewe kama kijenzi muhimu kwa elimu ya mtoto wako. Usiwahi kusita kutufikia kwa msaada wowote unaoweza kuhithitaji – **kwa kuwa tu washiriki.**

- **Dkt. Khalilah Campbell,**
*Afisa wa Umma Spesheli*

## UNAPOKUWA MKAAZI MPYA KWENYE SHULE MAREKANI…

**Wakala wa Uhamisho wa Wakimbizi wanaokubali mchango kusaidia familia mpya zilizowasili za Wakimbizi**

**Mashirika ya Imani mbalimbali**
713-533-4900

**Misaada ya Kikatholiki**
713-526-4611

**Huduma ya Muungano wa Tamaduni-anuwai**
713-776-4700

**Huduma ya Kimataifa ya YMCA**
713-339-9015

**Huduma za Wakimbizi wa Texas**
713-644-6224

# KURUNZI YA COOP ES




Mwaka 1950, Shule ya Msingi ya Coop ilijengwa na kupewa jina kwa heshima ya Ethel R. Coop, Mdhamini wa Baraza (1928-1942). Bi. Coop alianzisha desturi ambayo inaendelea kuishi kwa mojawapo ya Vyuo vinavyoongoza vya Uwili Lugha vya Houston. Leo, misheni ya Coop inaendelea kuwa, kuwa na wajibu wa kuendeleza kua kiakademiki na kibinafsi kupitia maendeleo ya uhusiano. Wanafunzi wanahimizwa kutengeza fursa na wanawezeshwa na vifaa kuwa wahitimu wa kimataifa. Coop ni mojawapo ya vyuo vya Uwili Lugha yenye fanaka wilayani. Programu hiyo inategemea utafiti na inafuata mihimili tatu muhimu: Uzungumzaji na ujuzi wa Lugha-Mbili, Ufanisi wa Kiakademiki, na uwezo wa Kitamaduni-jamii.

Fanaka ya programu ya Coop Uwili Lugha inajulikana kwa wilayaa yetu na kuwekwa nukuu na wataalamu wa programu. Wakati wa kuzuru Januari 2020, Dkt. Thomas na Dkt. Collier walikiri upatano wa mifumo na taratibu kuanzia kabla ya chekechea kufikia kidato cha tatu. Kilichonukuliwa kwa uwili na viongozi ni kiwango cha maelekezo makali na maagizo ya uandishi yanayozingatiwa kwenye vidato vyote kwa lugha zote mbili kwenye maeneo ya maudhui.




**Mwalimu mkuu wa awali, Tudon Martinez, ambaye sasa ni SSO wa Ofisi ya Shule ya Upili anasema hivi kuhusu Coop ES:**

Ninajivunia sana kwa mafanikio yote yanayofanyika kwenye Shule ya Msingi Ya Ethel R. Coop. Programu yetu ya Uwili Lugha inatambulika kama modeli ya programu ya HISD kama matokeo ya kazi ngumu, kupanga, kutekelezwa kwa uendeshaji bora, na uwajibikaji wa kikoa chetu kizuri cha Uwili Lugha. Walimu wetu wanafanya kazi kwa bidi kuhakikisha kuwa wametoa mazingira ya Uwili Lugha unaozingira vijenzi vyote vielelezi. Changamoto huwa katika kupata wakati, lakini ni jambo ambalo walimu hujitwika kushughulikia kingwana kwa kutanguliza kuongeza wakati wa maelekezo. Kwa hiyo, wanafunzi wetu wanahusishwa na wanawekwa kwenye njia ya ujuzi wa lugha mbili kila siku.

Kazi hii ngumu inafuatiliwa na kusaidiwa na juhudi za mratibu wetu wa Uwili Lugha, Bi. Nora Rubalcava, ambaye amekuwa jiwe la pembeni wa programu tangu uanzishaji wake. Amepita kutoka kuwa mwalimu wa Uwili lugha hadi kwenye jukumu la kuwa mratibu, akihakikisha kuwa maelekezo aliyotoa kama mwalimu ni sawia kwenye chuo.



Mwaka huu Jamii ya Coop inamkaribisha mwalimu mkuu Luis Sabillon. Anawajibika kuendelea na kazi nzuri ambayo walimu, wafanyakazi, na wasimamizi wamefanya kufanya chuo kiwe kizuri na kutoa sera ya mlango-wazi kwa wafanyakazi na wazazi. Bw. Sabillon analeta ukwasi wa ujuzi na maarifa, kwa kuwa amehudumia watoto na wazazi wa HISD kwa miaka 18. Majukumu yaliyopita ni ikiwemo kufanya kazi kama Mkuu wa Maelekezo wa Shule ya Marshall, ambapo alisaidia maelekezo ya ESL, kuwafunza walimu, na kuwezesha mazingira salama ya mafunzo kwa wanafunzi wote. Mbeleni katika kazi yake alifunza vidato vya nne na tano katika Shule ya Msingi ya Brookline.



Lengo kuu la Mwalimu Mkuu Sabillon kwa wasomi wa Coop ni kufanya kazi pamoja na wanafunzi na wazazi kutoa elimu bora kadri ya uwezo kwa wanafunzi. Amejitolea kuwapa wanafunzi fursa ya kua na kuwa bora kwenye darasa. Mwalimu Mkuu Sabillon anaaamini kuwa uwajibikaji unaohitajika kuendeleza wanafunzi wa kudumu waliokamilika kunahitaji jamii kufanya kazi pamoja.

***Mwalimu Mkuu: Luis Sabillon***
Baruapepe: ***LSABILLO@houstonisd.org***
***https://twitter.com/Coop_Eagles***
Baruapepe: ***CoopES@houstonisd.org***
***https://www.houstonisd.org/coopes*** ■

# KULEA MTOTO ANAYEONGEA LUGHA MBILI

**Huku shule zikifunguliwa, wazazi wana mara nyingine fursa ya kukutana na mwalimu wa mtoto wao, lakini, kabla ya kuingia kwenye kongamano la wazazi-walimu, andika orodha ya maswali na majibu. Ichukue nawe orodha hii. Haya hapa maoni ya kukuelekeza:**

- Je, nini kitafunzwa kwenye darasa lako mwaka huu?
- Je, ni kiwango gani cha kazi ya ziada wewe hupeana?
- Je, mtoto wangu atahitaji matayarisho gani kila siku kwa kazi ya siku?
- Masharti ya darasa na matokeo kutoyafuata ni gani?
- Je, kuna miradi mikubwa inayokuja? Je, utawajulisha wazazi vipi kuihusu?
- Je, mtoto wangu atakuwa na fursa zipi za kutangamana za mwanafunzi-kwa-mwanafunzi katika darasa lako?
- Je, utajuaje ujuzi wa mtoto wangu wa Kiingereza na ni misaada gani unaweka kuhakikisha kuwa wana fanaka kwenye darasa lako?
- Je, unafanya nini kumsaidia mtoto wangu kuboresha ujuzi wake wa Kiingereza?
- Je, nitahitajika kufanya nini nyumbani kumsaidia mtoto wangu kufanya vyema shuleni?

**Ndizo hizi mada ungetaka kuwa tayari nazo kwa mwalimu:**

- Masomo mtoto wako anayopenda (na asiyopenda).
- Mtoto wako hujifunza vipi vyema.
- Kinachompendeza mtoto wako nje ya shule.
- Hali za nyumbani zinazoweza kuathiri tabia za mtoto wako shuleni.



# KUSAIDIA WANAFUNZI WA KIINGEREZA HAPA TX

**Usaidizi wa Houston ISD**
Kozi Kuu:
***https://bit.ly/3thXK9M***
Ujumbe kuhusu mafunzo ya nyumbani na HISD

Orodha ya makazi ya Kifasihi:
***https://www.houstonisd.org/Page/184314***

**Nyenzo za Wazazi**
Usaidizi wa Wakala wa Elimu Texas:
***http://bit.ly/3t69k8k***n

**Tovuti muhimu za Kujifunza Nyumbani**
*Tovuti hizi zitasaidia katika kuimarisha Ujuzi wa Lugha ya Kiingereza: Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma, na Kuandika.*

Kiingereza: ***https://bit.ly/3sO9t0A***

Kihispania: ***https://bit.ly/38bMmmO***

**Watoaji Mtandao: Kuweka Utangamano wa Familia**
Kiingereza: ***https://bit.ly/2OteiN2***

Kihisipania: ***https://bit.ly/3mkfFtG***

Programu za Elimu na Ujuzi wa Watu Wazima
***https://bit.ly/3wqVOxl***

**Afya na Usalama –Mpango wa Marejeo ya Shule ya HISD**
***https://www.houstonisd.org/ReadySetGo***

**Cho Kikuu cha Wazazi**
**TENGA TAREHE**
VIPINDI VYA 2021-2022:

Jumanne, Sept. 14, 2021 - Wheatley HS
Jumanne, Oct. 19, 2021 - Scarborough HS
Jumanne, Nov. 16, 2021 - Milby HS
Jumanne, Jan. 18, 2022 - Madison HS
Jumanne, Feb. 15, 2022 - Bellaire HS
Jumanne, Apr. 19, 2022 - Houston MSTC

***https://www.houstonisd.org/ParentUniversity*** ■